**UGONJWA WA TAWAHUDI: TAARIFA YA UKWELI KWA WAZAZI**

**Ugonjwa wa tawahudi (ASD) ni nini?** Tawahudi ni ugonjwa unaodhoofisha ukuaji, au ujuzi na uwezo wa kufikiria. Unasababishwa na tatizo la jinsi akili hufanya kazi linadhoofisha uwezo wa mahusiano ya kijamii, mawasiliano na tabia. Tofauti hizi za akili zinaweza kusababisha matatizo kama vile tabia ya kujirudiarudia na matatizo ya mawasiliano. Mtoto aliye na ugonjwa wa tawahudi (ASD) ana matatizo ya mawasiliano na mwingilioano wa kijamii ambayo hayawezi kufafanuliwa na *kuchelewa* kwa ukuaji; mtoto ana msogezo wa kuvutiwa na taia za kujirudiarudia, tamaa, na shughuli, na pia anaweza kuwa na mjibizo usio wa kawaida kutokana na hisia.

**Ugonjwa wa tawahudi unabainishwaje?** Wataalamu walio na uzoefu wa kuchunguza ugonjwa wa tawahudi (ASD) huwahoji wazazi kuhusu tabia za mahusiano ya kijamii, mawasiliano na kucheza kwa mtoto wao, ukuaji wa lugha, na wanamkagua mtoto kwa dalili za kitabia. Wanalinganisha dalili za mtoto na orodha iliyoundwa na Shirika la Tiba ya Kiakili la Marekani. Wanaangalia kama tabia ya mtoto ni tofauti na umri wa mtoto huyo, au kama dalili zinaonyesha hali nyingine ya ukuaji. Lazima dalili zianze utotoni na lazima ziathiri utendaji wa mtoto wa kila siku. Ikiwa mtoto ana dalili za kutosha, basi mtoto huyo hutambuliwa kama mtoto aliye na ugonjwa wa tawahudi. Neno "spektra" humaanisha kwamba dalili za tawahudi (ASD) zinaweza kuwa dalili kidogo hadi dalili kali.

**Tawahudi husababishwa na nini?** Tunachojua: tawahudi huwa haisababishwi na wazazi! Tawahudi (ASD) ni ugonjwa wa ukuaji wa neva, jambo ambalo hutokea wakati wa ukuaji wa mapema wa akili. Pia tunajua kwamba ukaguaji wa mapema na matibabu ya mapema ni muhimu sana. Tawahudi (ASD) hujitokeza kwa namna nyingi zinazosababishwa na zaidi ya sababu moja. Zaidi ya 1% ya watoto au mtoto 1 kati ya watoto 88 Marekani wana tawahudi (ASD). Utafiti unaonyesha kwamba kuna jeni mbalimbali zinazosababisha tofauti za akili katika akili, lakini jinsi jeni hizo hunasababisha tawahudi (ASD) bado haieleweki. Bado watafiti wanachunguza sababu nyingine, kama vile mazingira na visababishi vingine. Kumtembelea mwanajenetiki kunaweza kusaidia kubainisha kama tawahudi (ASD) ya mtoto wako ina sababu mahsusi ya jenetiki.

**Huwa inapona?** Watoto wote walio na tawahudi (ASD) hukuza uwezo wao wa mahusiano ya kijamii, lugha na tabia baada ya mafunzo ya kina, yanayoanza mapema. Watoto wengi walio na tawahudi (ASD), hata wale ambao dalili zinapungua haraka, watakuwa na tofauti za maisha katika tabia na mawasiliano ya kijamii. Kumbuka kwamba kila mtoto ni tofauti na kwamba watoto wote walio na tawahudi (ASD) wana mahitaji na dalili tofauti.

**Tiba za tawahudi (ASD) ni kama gani?** Tiba za ukuaji na tabia ndio tegemeo kuu la tiba. Kwa watoto walio na matatizo makali ya mawasiliano na mwingiliano wa kijamii, lengo la tiba huwa kukuza tabia rahisi, kama vile kuashiria kitu kwa kidole au kuangalia kitu, na kuwasiliana kwa sauti. Mara kwa mara mtaalam wa matibabu humpa mtoto zawadi. Tiba hii hufanya vizuri zaidi wakati wazazi wanajifunza na kutumia mbinu hizo hizo na mtoto wao. Kwa watoto walio na dalili kodogo, kuna tiba nyingine ambazo husaidia kumfunza mtoto uwezo wa lugha na mahusiano ya kijamii. Programu ya tiba na kielimu ni bora wakati inaongozwa na mtu au timu iliyo na uzoefu wa tawahudi (ASD).

**Ninaweza kufanya nini ili nimsaidie mtoto wangu?** Endelea kufanya mambo yote mazuri unayofanya kama mzazi. Uliza ufundishwe baadhi ya mbinu za tiba ili uweze kuzifanya na mtoto wako. Jifunze mengi uwezavyo kuhusu uaguzi wa mtoto wako ili uwe mmoja wa timu ya mtoto wako aliye na ujuzi. Omba nafasi ya kupumzika ili uweze kuwa na nguvu ya kuwa mzazi na pia mwalimu maalum kwa mtoto wako. Shirikiana na familia nyingine ili mshirikiane mikakati na nyenzo.

**Kuna dawa zinazoweza kusaidia?** Kwa wakati huu, hakuna dawa zinazoweza kutibu tawahudi (ASD). Watoto walio na tawahudi (ASD) wanapokua wanaweza pia kuwa na dalili za wasiwasi au mfadhaiko. Watoto wengine wanaweza kuwa na tabia ya kijiumiza, tabia za kujirudiarudia na tamaa, au kutomakinika, mihemko na kupepesuka

(ADHD). Wakati mwingine daktari wa watoto au daktari wa akili wa watoto anaweza kupunguza dalili hizi kwa kutumia dawa.

**Je, mtunzaji wa karibu wa mtoto wangu anaweza kufanya nini kusaidia?** Daktari wako wa watoto au mtunzaji wako wa karibu ("tiba nyumbani") anaweza kukusaidia:

- kufuatilia matatizo ya kimatibabu yanayoweza kutoka mara nyingi kwa watoto walio na tawahudi (ASD)
- kupanga huduma ya kimatibabu na miadi ya mtoto wako
- kufanya uamuzi kuhusu chaguo za tiba na kutoa mapendekezo ikiwa kuna changamoto kubwa za tabia, wasiwasi, au usununu.
- kuagiza matibabu yanayosimamiwa na bima katika Vermont kwa sasa
- kushiriki katika mikutano ya timu ya mtoto wako
- kutetea mahitaji yako kama familia kuhusu utunzaji wa mtoto wako

**Je, mtoto wetu anafaa kuonekana katika Kliniki ya Ukuaji wa Mtoto tena?** Tunaweza kufanya mpango mahsusi wakati wa miadi ya mtoto wako ya CDC mrudi kwa ukaguzi au utathmini zaidi. Pia tunapatikana wakati wowote kujibu maswali au masuala yako; na pia unaweza kuitisha ziara ya kufuatilia. Wakati watoto wana ukaguaji ulioanzishwa na programu nzuri ya tiba huwa hakuna haja kubwa ya kufuatilia timu ya CDC.

**Nani mwingine anaweza kunisaidia?** Tiba ya mapema kwa mtoto wako, elimu ya mapema au timu ya elimu maalum katika shule ya mtoto wako, na pia watoa huduma kutoka uajenti wa huduma ya ukuaji katika jamii yako wanaweza kukusaidia. Mikutano ya mara kwa mara na timu ya mtoto wako inaweza kusaidia sana. Wazazi wengine wa watoto walio na tawahudi (ASD) na makundi ya kuwatetea wazazi kama vile Vermont Family Network, yanaweza kutoa mawazo mengi mazuri na usaidizi kwa familia. Taarifa na nyenzo zaidi, ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu jinsi ya kufikia bima ya tawahudi kwa watoto wa VT, na viungo vya mashirika ya kitaifa inaweza kupatikana katika www.vermontfamilynetwork.org/i-need-help-with/developmental-disabilities/autism/.

Pia tunapendekeza vitabu na tovuti zifuatazo zinazoaminika:

- The Autism Speaks 100 Day Kit ilianzishwa haswa kwa familia zilizobainisha kwa mara ya kwanza ili kuwasaidia kutumia vizuri iwezekanavyo siku 100 zinazofuata uaguzi wa tawahudi (ASD): www.autismspeaks.org/docs/family_services_docs/100_day_kit.pdf
- Tovuti ya The National Professional Development Center ina taarifa kuhusu tiba 24 za ushahidi za kuwafunza watoto walio na tawahudi (ASD): http://autismpdc.fpg.unc.edu/content/briefs
- The Center for Disease Control and Prevention ASD fact sheet : http://www.cdc.gov/ncbddd/actearly/pdf/parents_pdfs/autismfactsheet.pdf
- *Sound Advice on Autism* , mkusanyiko wa mahojiano kupitia Akademia ya Madaktari wa Watoto ya Marekani (AAP) ya wazazi yanayowahusisha madaktari wa watoto, watafiti na wazazi kusaidia kujibu maswali ya wazazi kuhusu tawahudi (ASD): http://www.aap.org/audio/autism/
- The Vermont Next Steps Guide kina taarifa muhimu na nyenzo kutoka jimbo lote kwa familia za VT zilizo na watoto walio na tawahudi (ASD):http://www.ddas.vermont.gov/ddas-publications/publications-autism/publications-autism-documents/next-steps-autism
- Kwa msaada wa kulipia vifaa, vidude maalum vya kuchezea watoto, au huduma za watoto wa VT walio na tawahudi (ASD) tuma maombi kwa Autism Puzzle Foundation: www.vtautismpuzzle.org
- Autism Spectrum Disorders: What Every Parent Needs to Know, kilichohaririwa na Alan Rosenblatt, MD, Paul Carbone,MD, na Winnie Yu, kilichochapishwa na Akademia ya Madaktari wa Watoto ya Marekani, 2013.

- Making Sense of Autism Spectrum Disorders: Create the Brightest Future for Your Child with the Best Treatment Options, kilicho andikwa na James Coplan, MD, Bantam Books, NY, 2010.

Taarifa hii ya ukweli iliandikwa na tephen H Contompasis MD, Carol Hassler, MD, na Janet Kilburn, LICSW kwa usaidizi kutoka kwa *Ruzuku ya Utekelezaji wa Jimbo wa Uboreshaji wa Watoto na Vijana walio na Tawahudi (ASD) na Malemavu mengine ya Ukuaji* ya Vermont